

Msamaha wa Sheria ya Vikwazo Waiver of Statute of Limitations

Kila mwezi wa msaada wa watoto ambao haujalipwa utakuwa na hukumu. Sheria ya vikwazo huweka kipindi cha muda ndani ya kipindi ambacho hukumu inaweza kutekelezwa au kukusanywa. Baada ya sheria hio ya vikwazo kuanza kazi, deni hilo "huisha muda wake" na haiwezekani kutekelezwa tena. Sheria ya vikwazo ya deni la msaada wa watoto inaweza kutegemea vigezo mbalimbali, kama vile tarehe ya agizo la msaada ilipotoandikwa, wapi agizo la msaada limeandikwa, na ni jimbo gani hatua ya utekelezaji inafanyika. Unaweza kuhitaji kutafuta ushauri wa kisheria juu ya hali ya deni lako la msaada na sheria ya vikwazo ambayo itatumika katika agizo lako la msaada.

MSAMAHA

Katika kuzingatia mpango wa malipo uliopunguzwa au ulioahirishwa, Nakubaliana na kusamehe sheria yoyote ya ulinzi wa vikwazo katika ukusanyaji wa msaada wa watoto ninaodaiwa. Ikiwa nadaiwa na mwenzi msaada wa mzazi mwingine wa watoto wowote waliotajwa katika msamaha huu, msamaha pia utaathiri msaada wa mwenzi unaodaiwa kwa mzazi huyo. Msamaha huu unaathiri deni langu la msaada kwa watoto wanaofuata:

Msamaha huu utatumika kwa:

1. Deni lolote la msaada ambalo ni la sasa au mbeleni. Hii inajumuisha msaada wa watoto, msaada wa matunzo ya watoto, msaada wa matibabu, na msaada wa mwenzi (masurufu) ikiwa imeagizwa na ikiwa DCS inatekeleza agizo langu la msaada wa watoto.
2. Sheria yoyote ya ulinzi wa vikwazo iliyoundwa na RCW 4.16.020, RCW 4.56.210, au RCW 6.17.020.
3. Sheria nyingine yoyote ya jimbo la Washington au sheria ya jimbo jingine ambalo linazuia muda ambao DCS inaweza kukusanya deni langu la msaada.

Msamaha huu haurudishi hukumu zozote kwa sasa zilizozuiwa na sheria yoyote. DCS haiwezi kukusanya deni lolote la msaada ambalo tayari limepotea kwa sheria ya vikwazo. Msamaha huu hauniruhusu kulipa chini zaidi ya jukumu langu kamili la sasa la msaada.

Msamaha huu unairuhusu DCS kukusanya kutoka kwangu mpaka nitakapolipa deni langu la msaada kikamilifu. Msamaha huu utalinda deni la msaada lisipotee kutokana na sheria ya vikwazo lakini hauzui ulinzi mwingine wowote. RCW 74.20A.220 inaniruhusu kufanya msamaha huu.

Msamaha huu utaendelea kubakia katika utekelezaji mpaka DCS itakapo toa kwa maandishi.

Imesainiwa katika _____, Washington.

TAREHE

SAINI

Rejesha kwa:
DIVISION OF CHILD SUPPORT
PO BOX 11520
TACOMA WA 98411-4420
Faksi: 866-668-9518

Katika kujibu, taja nambari za kesi:

Hakuna mtu kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya uraia, imani, dini, jinsia, umri, au ulemavu, atapaswa kupaguliwa dhidi ya kutopata ajira, huduma, au sehemu ya shughuli za programu. Fomu hii inapatikana katika miundo mingine kulingana na ombi.